KENYATTA UNIVERSITY

EXAMINATION FOR THE DEGREE OF BACHELOR OF ARTS

CCM 103: KISWAHILI FOR MASS COMMUNICATION

2ND SEMESTER 2024/2025 TIME: 2 HOURS

**MAAGIZO:**

- **Jibu Maswali MATATU.**
- **Swali La KWANZA ni La LAZIMA.**

1. a) Eleza changamoto zinazokumba matumizi ya Kiswahili katika vyombo vya habari vya kitaifa na kimataifa. (alama 12)

   b) Wewe ni mwanahabari unayefanya kazi katika kutafsiri makala kutoka lugha ya Kiingereza hadi lugha ya Kiswahili katika runinga ya Mwanaspoti. Fafanua changamoto ambazo unaweza kukumbana nazo katika mchakaato huu. (alama 10)

   c) Kwa kutolea mifano mwafaka, fafanua aina mbali mbali za maneno ya Kiswahili ambayo wewe kama mwanahabari unaweza kutumia katika kuandika makala katika vyombo vya habari. (alama 08)

2. Katika tasnia ya uanahabari, tafsiri na fasiri ni jambo la kimisingi. Fafanua aina zifuatazo za tafsiri na uzitolee mifano mahususi.

   a) Tafsiri ya Kisemantiki (alama 10)

   b) Tafsiri ya kimawasiliano (alama 10)

3. a) Wewe kama mwanahabari unayefanya kazi katika kituo cha runinga cha Mwaminifu TV, umeteuliwa kumhoji Waziri wa Habari na Mawasiliano kuhusu nafasi ya Kiswahili katika tasnia ya uanahabari. Fafanua matayarisho utakayoyafanya kabla ya kumhoji waziri. (alama 10)

   b) Kwa kutolea mifano mwafaka, onyesha ni kwa namna gani lugha ya Kiswahili inatumiwa katika mawanda ya kimataifa. (alama 10)

4. a) Fafanua sifa mbali mballi za lugha tandawazi. (alama 10)

   b) Pambabua hatua au mchakato ambao wewe kama mhariri unapaswa kuufuata ili kuibuka na makala safi yaliyohaririwa. (alama 10)

*INVOLVEMENT IN ANY EXAMINATION IRREGULARITY SHALL LEAD TO DISCONTINUATION*

5. a) Onyesha ni kwa namna gani matumizi ya Kiswahili katika mitandao ya kijamii yanaweza kuongeza na kuchangia mipaka ya kitabaka katika jamii.

(alama 8)

b) i. Tambua vigezo viwili vikuu ambavyo hutumiwa katika kuainisha sentensi za Kiswahilii. (alama 4)

ii. Kwa kutolea mifano mwafaka, pambanua aina nane za sentensi za Kiswahili ambazo wewe kama mwanahabari unaweza kuzitumia katika kuandika makala katika gazeti. (alama 8)